UJUMBE KWA SERIKALI

Kuratibu Ulinzi wa Watoto kipindi cha Kukabiliana na COVID-19

Ujumbe wa Jumla

COVID-19 ni dharura ya kiafya ya umma yenye madhara mengi ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja katika usalama wa watoto, ustawi, na maendeleo yao, kwa muda mfupi na kwa muda mrefu. Kwa mfano, kufungwa kwa shule, kuwekwa kizuizini, na kupungua kwa usalama wa chakula na mapato ya kaya huweka maisha ya watoto katika hatari, kama ukatili, unyonyaji, unyanyasaji, kutengwa na familia na njia hatarishi za kukabiliana za kifamilia, kama ndoa za utotoni and ajira hatarishi kwa watoto.

Kwa hivyo, mikakati ya Ulinzi wa Watoto inaokoa maisha ya watoto. Mipango ya kujiandaa na kukabiliana na COVID-19 inapaswa kuhusisha huduma za ulinzi kwa walio hatarini zaidi ili kuhakikisha kuwa hatua za ulinzi za kuokoa maisha zipo na zinapatikana kwa watoto na familia zao.

Kuchukua mkakati mzima wa serikali na kuuratibu na wizara zinazo husika ni muhimu katika kuhakikisha mfumo kamili wa sekta mbalimbali unaohakikisha watoto wanalindwa katika maeneo yote ya maisha yao.

Hatua zote za kuwalinda watoto katika kukabiliana na COVID-19 zinapaswa: kuendana na Viwango vya chini vya Ulinzi wa Mtoto katika Hatua za Kibinadamu; kulenga ushiriki wa watoto; na kuwa shirikishi, ukizingatia jinsia, umri, ulemavu, na tofauti zingine.

Ulinzi dhidi ya Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (PSEA) unapaswa kuhusishwa katika kukabiliana na COVID-19, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ufikiaji salama kwenye huduma zote na mifumo ya kuripoti kesi yenye usiri, na rafiki kwa mtoto.Kwa maelezo zaidi, angalia Muongozo wa Kitaalamu wa muda wa Kamati ya kudumu ya Asasi mbalimbali juu ya Kuzuia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia wakati wa kukabiliana na COVID-19.

HATARI ZA KUTOKUWEKA KIPAUMBELE KATIKA MIKAKATI YA ULINZI WA MTOTO KIPINDI CHA JANGA LA COVID-19

- Kesi za ulinzi wa mtoto zenye hatari kubwa kuachwa bila ufuatiliaji au mipango mbadala.
- Kesi mpya za ulinzi wa mtoto hazizingatiwi au kupewa rufaa ipasavyo.
- Hatari za ulinzi wa mtoto ambazo mara nyingi hufichwa, kama unyanyasaji wa kijinsia, ukatili wa kimwili, au kutelekezwa, hazita gundulika bila wafanyakazi wa ulinzi wa mtoto kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mar na usimamizi.
- Watoto zaidi wanawekwa katika hatari, kama wale waishio mitaani, waliotengwa kutokana na ugonjwa katika familia au hatua zingine zinahusiana na COVID-19 kama kuwekwa karantini au zuio la kusafiri.
- Kupungua kwa uwekezaji wa serikali kwenye huduma za kijamii na upatikanaji wa huduma kupungua sana (mf. Kutokuwekwa kwa huduma za kutokea mbali za kuwasaidia watoto waliopo majumbani).

Ujumbe Maalumu

1. Weka kipaumbele katika Ulinzi wa Watoto

- Serikali lazima ziainishe na kuwahudumia watoa huduma za kijamii kama wafanyakazi muhimu kipindi cha mlipuko wa COVID-19, kuwaruhusu kuendelea kutoa msaada wa kuokoa maisha ya watoto na familia.

- Badilisha programu zilizopo kulingana na ugumu wa ufikiaji, kwa mfano kuimarisha simu ya msaada kwa watoto, ujumbe kwa njia ya redio, kuanzisha ufuatiliaji kutokea mbali na kesi za watoto walio katika mazingira magumu, etc.

- Weka kipaumbele katika huduma za ulinzi wa mtoto, ikihusisha msaada wa afya ya akili na wakisaikolojia, usimamizi wa kesi, huduma za melezi mbadala na usimamizi, simu za msaada kwa watoto, na huduma nyingine za muhimu, kati ya huduma za msingi ili hizi huduma za muhimu ziendelee kutolewa.

- Wasaidie wasimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto kuendeleza na kuboresha msaada kwa watoto na familia zilizo katika hatari kubwa ya ukatili, unyanyasaji na unyonyaji. Zipe kesi kipaumbele kulingana na kiwango cha hatari (mf. Kesi zenye hatari kubwa, kati, na chini) na ubainishe hatua zinazopaswa kuchukuliwa kulingana na kiwango cha hatari. Tazama ukurasa wa pili wa mfano wa muongozo wa Usimamizi wa Kesi za Ulinzi wa Mtoto kwenye COVID-19 nchini Lebanon . *Muongozo katika ngazi ya Dunia unakuja.*

- Shirikiana na mashirika ya asasi za kiraia na sekta binafsi kuziba pengo katika ufadhili na nguvu kazi ya huduma za kijamii.

- Kwa kuweka jukwaa la uratibu, mamlaka husika na wizara zinazo husika zinapaswa kufanya kazi na mashirika na taasisi za ulinzi wa mtoto katika ngazi mbalimbali ili kuongeza rasilimali za pamoja na kuboresha ufanisi na ubora wa kukabiliana kwa ujumla.

2. Watoto walio hatarini katika karantini au waliotengwa

- Tekeleza itifaki na mipango ya kuwatenga au kuwaweka karantini watoto wanaougua ambayo itawawezesha kuendelea kupata mahitaji yao ya kimwili na kiakili wakati wa COVID-19. Wezesha itifaki ziruhusu wazazi kukaa na watoto wagonjwa pale inapowezekana.

- Pale ambapo wazazi na watoto wametengana kwa muda na mlezi wa msingi, wezesha mawasiliano ya kila mara kupitia kuongea na simu, ujumbe wa video, n.k.

- Hakikisha kunakuwa na njia mbadala za malezi za kifamilia kwa watoto ambao walezi wao wapo karantini, huku malezi ya

muda mfupi yasiyo ya kifamilia (mf. Kikundi kidogo nyumbani au kituo cha malezi cha muda mfupi) yakiwa chaguo la mwisho.

3. *Afya na Ustawi wa Wafanya kazi*

- Wapatie wasimamizi wa kesi na mafanyakazi wa jamii vifaa muhimu vya kujikinga na mafunzo ya kukabiliana na hatari ili kuendelea kutoa huduma muhimu *kwa usalama,* katika kusaidia malezi na usalama wa watoto katika jamii.
- Weka miongozo ya maambukizi, uzuiaji na udhibiti (IPC) kwa wafanyakazi wa kesi kuhakikisha afya na usalama wa watoto/walezi, wasimamizi wa kesi na wanajamii wanaojitolea.
- Bainisha njia za kuunda mitandao mipya au sehemu za mtandaoni ili wafanyakazi wa kijamii waweze kupata habari na marafiki na mitandao mingine ya msaada na kuwapatia teknolojia na vifaa vinavyohitajika kufanya hivyo.
- Hakikisha watoto wanaowatunza / kuishi na walezi wazee au walezi wenye ugonjwa hatari au ulemavu wanapewa kipaumbele kwa msaada wa haraka.

4. *Ushirikiano wa Sekta Mbalimbali*

- Hamasisha ujumbe thabiti na sahihi kuhusu COVID-19 na njia za kupunguza athari kwa watoto (mf. kuhamasisha jumbe za malezi na njia chanya za kukabiliana, jinsi ya kupunguza hatari ya kutengwa na familia, n.k.) kwa kuratibu jumbe kati ya ulinzi wa watoto, ukatili wa kijinsia, afya ya akili, na watendaji wa afya.
- Kuboresha na kuimarisha njia za rufaa za sekta mbalimbali ili kuendana na huduma *mpya au zilizoboreshwa* za afya, elimu, afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, na husuma au rasilimali zingine.

Cover Photo Credit:
© UNICEF/UN0339412/Frank Dejongh

Aprili 2020

Badilishana na Jifunze

Mafunzo kutoka kwenye nchi yako ni ya muhimu. Kutazama rasilimali zilizopo and na kutushirikisha nyenzo, tafadhali rejelea Orodha ya Rasilimali ya Sehemu ya Majukumu ya Ulinzi wa Mtoto katika COVID-19 na wasiliana na dawati letu la msaada kupitia cpaor@unicef.org ili kuchangia. Kwa muongozo zaidi, angalia andiko la kiufundi la *the Alliance "Ulinzi wa Watoto kipindi cha janga la COVID-19" linalopatikana katika lugha 11: https://alliancecpha.org/en/series-of-child-protection-materials/protection-children-during-covid-19-pandemic*